HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE TOLEO LA 13 OKTOBA 2025

# Jarida la TEMEKE YETU



## ZIARA YA MHE, KWAGILWA KATIKA MIRADI YA MAENDELEO MANISPAA YA TEMEKE





www.temekemc.go.tz

Haliuzwi

# UTANGULIZI



**Ndg. Jomaary Mrisho Satura**
Mkurugenzi Manispaa ya Temeke

## TIMU YA UTAYARISHAJI

**Mhariri Mkuu**
Joanita Joseph

**Wahariri Wasaidizi**
Mussa Chisongela
Ramadhani Fupi
Sadam Ndemo

**Msanifu wa Jarida**
Abdulhamidu Shabani

**Wapiga Picha**
Gervas Edick
Simon Joshua
Ramadhani Fupi
Mussa Chisongela

**Jarida hili hutolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,**

Halmashauri ya Manispaa
ya Temeke
S.L.P 46343
Temeke,
Dar es Salaam
Simu: +255 22-2928132,

## IFAHAMU TEMEKE

Manispaa ya Temeke ni moja ya Halmashauri chache kongwe zenye utajiri na historia ambayo imechangia kuleta mabadiliko kisiasa, kiuchumi na kijamii Nchini.

Kwa ujumla Temeke imekuwa kitovu cha upatikanaji wa uhuru wa Tanzania bara, pia kwa ukuaji wa michezo, utamaduni na maendeleo ya kilimo katika jiji la Dar es Salaam.

Manispaa ya Temeke ina eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 240 iliundwa 1999 chini ya sheria ya Serikali za mitaa (mamlaka ya miji) ya mwaka 1982 Manispaa ya Temeke ipo kusini mwa mkoa wa Dar es salaam ambapo Mashariki inapatikana Bahari ya Hindi, Kusini inapakana na wilaya ya Mkuranga iliyopo mkoa wa Pwani na Kaskazini-Magharibi imepakana na manispaa ya Ilala wakati kwa upande wa Kaskazini-Mashariki Halmashauri hii imepakana na halmashauri ya manispaa ya Kigamboni.

Temeke ina majimbo makuu mawili ya uchaguzi (Temeke na Mbagala) ina idadi kubwa ya watu ambapo kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 idadi ya watu ni 1,346,674 kati yao wanawake ni 691,537 na wanaume ni 655,137.

Temeke ni moja ya Wilaya inayolibeba Jiji la Dar-es-Salaam, kivipi, Dar-es-Salaam ni Temeke kwa kuwa bandari ipo Temeke,viwanja vyote vya mipira kitaifa - Uwanja wa Taifa na uwanja wa Uhuru, pia ipo jirani na Uwanja wa ndege wa kimataifa, ni mwanzo wa Reli ya Tazara, ina Uwanja wa kimataifa wa maonesho - sabasaba, ina daraja la Nyerere ambalo ni la Kimataifa. Samaki hupatikana kwa uwingi,

Temeke, ina fukwe nzuri za kuvutia zenye mchanga mweupe, ina wakazi wengi na wahamiaji wanaopata maeneo ya kujenga kutokana na kuwa na maeneo makubwa tena ya wazi. Ina mtandao mkubwa wa barabara za lami.

Manispaa ya Temeke ni lango la kuingia kutoka Nchi za Kusini mwa Afrika zikiwemo Msumbiji, Afrika ya Kusini n.k kupitia upande wa Kusini upande wa Kaskazini kuna Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere hivyo ni rahisi kwa wawekezaji kufanya biashara za Kimataifa.

**Hii ndiyo Temeke tunayoisema.**

Nukushi: +255 22-2928137 Baruapepe:
temeke@temekemc.go.tz
Tovuti: temekemc.go.tz.



# MHE. KWAGILWA AIPONGEZA MANISPAA YA TEMEKE KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Na Joanita Joseph TMC Habari.**

"Nimeona Mnapanga kujenga Mradi huu kwa Miaka miwili, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya kwa Niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Tamisemi Profesa Shemdoe Nikuelekeze shule hii usijenge kwa Miaka 2. Watoto wa Chamazi wana uhitaji na eneo la kusoma. Kaeni upya na mje na muda sahihi unaozingatia uharaka wa shule hii kukamilika".

**"Lakini si tu hivyo, Shule hii ni Shule ya Sekondari kwahiyo katika namna mnavopangilia Ujenzi wenu, linapofika hitimisho la Shule kukamilika na Maabara ziwe zimekamilika".**

Moja ya Maelekezo aliyotoa Mhe. Reuben Kwagilwa leo Desemba 22, 2025 katika Ziara yake Manispaa ya Temeke. Mradi wa Shule Mpya ya Sekondari Mwembebamia, Kata ya Chamazi unatarajiwa kugharimu Kiasi cha Shilingi Bilioni 1.7 mpaka kukamilika kwake.

**Ikiwa ni Jengo la Sakafu 4, Madarasa 16 , Ofisi 8, na Vyoo 48.**



## DC MAPUNDA AHITIMISHA MAFUNZO YA WAJUMBE WAPYA BODI YA AFYA TEMEKE

**Na Mwandishi wetu, TMC Habari**

**Mkuu wa wilaya ya Temeke Mhe. Sixtus Mapunda Novemba 19, 2025 amehitimisha Mafunzo ya Wajumbe wapya wa Bodi ya Afya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke pamoja na Wajumbe wa Kamati za Afya za vituo vyote 31 vya kutolea huduma za Afya vya Umma vilivyopo katika Manispaa hii.**

**DC Mapunda amewataka wajumbe hao kuwajibika vyema katika kazi zao ili kuboresha utoaji wa huduma za afya katika jamii kwani wao ndio daraja kati ya wananchi na vituo vya kutolea huduma za Afya.**

**Mafunzo hayo yamelenga kuwapatia uelewa juu ya majukumu yao ikiwemo uwajibikaji, usimamizi wa fedha, ununuzi, utawala bora na katika sekta ya afya, n.k yakiratibiwa na Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Huduma ya Lishe Manispaa ya Temeke**





## MHE, UZAIRU ATOA NENO BAADA YA KUCHAGULIWA KUWA MEYA TEMEKE

**Na Mwandishi wetu, TMC Habari**

Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Mhe. Uzairu Abdul Athumani amewaagiza Watumishi wote wa Manispaa hiyo kutekeleza kikamilifu na kwa wakati ahadi zote zilizotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mhe. Uzairu ameyasema hayo Desemba 3, 2025 wakati akizungumza na waandishi wa Habari mara baada ya kumalizika kwa Mkutano wa kwanza wa Baraza la Madiwani uliofanyika kwenye Ukumbi wa Iddy Nyundo uliopo Manispaa ya Temeke.

Aidha Mhe. Uzairu amesema kwamba kwa upande wake kwa kushirikiana na Madiwani wamejipamga kuhakikisha kuwa wanasimamia ipasavyo rasilimali zote za Manispaa hiyo ili kuijenga Manispaa hiyo kuwa ya kisasa zaidi.

Kwa upande wake Naibu Meya wa Manispaa ya Temeke Mhe. Nuru Bayingana amewaomba wananchi kuwa wavumilivu akidai kuwa watahakikisha wanawapatia furaha wananchi kama alivyoagiza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan.

Pia, wananchi waliohudhuria Mkutano huo wa Baraza la Madiwani wameelezea imani yao kwa viongozi hao wapya wa Manispaa ya Temeke wakisema kuwa wanaamini kupitia viongozi hao Manispaa ya Temeke itaimarika zaidi.



## MKURUGENZI TEMEKE AELEZA MIRADI INAYOTEKELEZWA MBELE YA MADIWANI

**Na Joanita Joseph, TMC Habari**

Mkugenzi wa Manispaa ya Temeke Ndg. Jomaary Mrisho Satura akiwasilisha kwa Madiwani shughuli zilizotekelezwa na Manispaa katika Kipindi cha Julai hadi Novemba, 2025 sambamba na Miradi Mikubwa ya kimkakati iliyoanza kutekelezwa na inayotarajiwa kuanza kutekelezwa katika Mwaka wa fedha 2025/2026.

Mkurugenzi ametoa picha kwa Madiwani kubwa wa Manispaa ya Temeke, idadi ya Watu na Mpango na Bajeti ya Halmashauri kwa Mwaka wa fedha 2025/2026 sambamba na Lengo la Makusanyo ya Mapato ya halmashauri kutoka katika Vyanzo vyake vya ndani (Mapato ya Ndani) kwa Mwaka wa fedha 2025/2026.



MD Satura amewaomba Waheshimiwa Madiwani Ushirikiano katika Ukusanyaji wa Mapato ili kuwezesha Uendeshaji wa halmashauri na Utekelezaji wa Miradi hiyo mikubwa ya Maendeleo vinakwenda kufanikiwa jambo litakaloleta tabasamu kwa Wananchi na kufanya Temeke yetu kuwa ya Viwango.

# FEDHA HIZI MNAZOKWENDA KUKOPESHWA ZIMEPATIKANA KWA JASHO, NENDENI MKAZITUMIE KWA USAHIHI"- MD SATURA

**Na: Ramadhani Fupi, TMC Habari**

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii leo Desemba 19, 2025 imehitimisha Mafunzo maalumu kwa Vikundi 237 kundi la wanawake, vijana na watu wenye Ulemavu wanaotarajia kukopa Mikopo ya Asilimia 10 ya Mapato ya ndani ya halmashauri wenye thamani ya Shilingi Bilioni 7,517,146,645 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**VIKUNDI VITAKAVYONUFAIKA**

**237**

Akifunga Mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke Ndg. Jomaary Satura amesema kuwa fedha hizo ni za Mkopo zikitolewa kwa Wananchi bila riba na kusisitiza kuwa fedha hizo zimepatikana kupitia Jasho la Watu hivyo amewashi wanufaika wote wa Mkopo kutumia fedha hizo kwa usahihi.

"Fedha hizi mnazokwenda kukopeshwa ambazo hazina riba yoyote ni sehemu ya makusanyo ya asilimia Kumi ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ambazo tunazikusanya kutoka kwa Mama Ntilie, Muuza Ndizi na Bodaboda, tukikukabidhi wewe fedha za namna hiyo wewe ukienda kutumia kwa matumizi mengine sidhani kama utabaki salama, fedha hizi zimepatikana kupitia watoka jasho ", alisema Ndg. Satura.

Kwa upande wake Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Bi. Furaha Chiwile amewataka wanufaika wa Mkopo kuimarisha ushirikiano na upendo baina yao ili kudumisha amani na mshikamano katika jamii.

"Mnatakiwa mpendane, mtu anaweza kukuudhi lakini kwa manufaa ya jamii lazima ufanye nae kazi, twendemi tukatengeneze amani kwenye makundi yetu", alisema Bi. Chiwile.

Kwa upande wa wanufaika wa mikopo waliohudhuria Mafunzo hayo wameushukuru Uongozi wa Manispaa ya Temeke kwa Mafunzo hayo kwani yamewaongezea uwezo wa kutumia vyema mkopo huo na kuahidi kuwa watatumia mkopo huo kwa usahihi ili kufikia malengo yao.





# BARAZA JIPYA LA MADIWANI MANISPAA YA TEMEKE 2026
















# MADIWANI WAMCHAGUA MEYA, NAIBU MEYA TEMEKE

**Na Abdulhamidu Shabani, TMC Habari**

Baraza Jipya la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Temeke limekutana Desemba 3, 2025 na kumchagua Mhe. Uzairu Abdul Athuman kuwa Mstahiki Meya huku Mhe. Nuru Cassian Bayingana akiwa Naibu wake.

Tayari Madiwani wameunda Kamati za kudumu na zisizo za kudumu kwa Mujibu wa Kanuni na Sheria na kuchagua Wenyeviti wao, huku Mstahiki Meya Uzairu akitoa Dira na Mwelekeo wa Baraza analolitaka akiahidi kuiongoza Manispaa ya Temeke kuwa ya Viwango na Kisasa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Utekelezaji wa Ahadi za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alizozitoa ndani ya siku 100 toka alivyoapishwa zinafanyika, kusimamia Matumizi sahihi ya Rasilimali fedha na watu ndani ya halmashauri, kusimamia Mipango na utekelezaji wa Miradi ya maendeleo, uwezeshaji wa Vijana katika kuwapatia fursa za ajira, Mikopo na utekelezaji wa Mipango ya Wizara mpya ya Vijana.

Kwa upande wake Katibu Tawala Msaidizi Ukaguzi na Ufuatiliaji Mkoa wa Dar es salaam amebainisha kuwa Temeke ni miongoni mwa Injini ya uchumi katika Mkoa wa Dar es salaam hivyo kutoa Wito kwa Madiwani kusaidiana na Mkurugenzi kukusanya mapato, kusimamia Watumishi na kuepuka migogoro inayotokana na kutofuata Sheria na taratibu.






# CRDB BANK YAKABIDHI MADAWATI SET 30 KWA AJILI YA SHULE YA SEKONDARI DOVYA

**Na: Abdulhamidu Shabani, TMC Habari**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Ndg. Jomaary Mrisho Satura Novemba 25, 2025 amepokea jumla ya set 30 za Madawati (Viti na Meza) kutoka Benki ya CRDB ikiwa ni utaratibu wa Benki hiyo kurudisha Sehemu ya faida yake kwa jamii hususani katika Sekta ya Elimu, Afya na Mazingira.

Akizungumza katika hafla hiyo fupi MD Satura ameishukuru Benki ya CRDB kwa kuiwezesha Manispaa ya Temeke kuwa sehemu ya Watanzania walionufaika na CRDB kupitia utaratibu huo huku akitoa Wito kwa Benki hiyo kuendelea kugusa Manispaa ya Temeke kila zinapotokea fursa hizo hasa katika Sekta ya Elimu na Afya.

"Temeke ni halmashauri inayoongoza kwa idadi kubwa ya watu na mzunguko mkubwa wa kibiashara kwakuwa mmekuwa wadau wazuri tunawashukuru na tunaendelea kufungua milango ya mashirikiano tuko tayari kushirikiana na ninyi, tunafahamu mchango mkubwa wa CRDB kwenye ukuaji wa Biashara za Wananchi wetu na ukuaji wa pato la Taifa, tunawapongeza sana. Nashukuru tunaishi kama familia na CRDB Bank, Mungu awabariki" alisema MD Satura

AKikabidhi Madawati hayo Meneja wa CRDB Tawi la Taifa Bi. Edna Mauya amesema

"CRDB Bank tumekuwa na utaratibu wa kurudisha Asilimia moja ya pato zetu tunazopata kwa jamii na kupitia programu yetu ya "Keti Ujifunze" tunajua kwenye shule zetu tuna uhitaji mkubwa wa madawati, kulingana na situation hiyo tukasema na sisi CRDB tuchangie hivyo leo tunakabidhi Madawati Set 30 kwa ajili ya Shule ya Sekondari Dovya" Alisema Bi. Edna

Kwa upande wake Mkuu wa Shule ya Sekondari Dovya Ndg. Mohamed Juma Ally amesema Madawati haya ni chachu na itakuwa ni muendelezo wa Ukuaji wa taaluma Shuleni hapo.

# BODI YA MICHEZO YA KUBAHATISHA TANZANIA (GBT) YATOA MSAADA WA MADARASA NA MADAWATI SHULE YA MSINGI RUFU.

**Na: Simon Joshua, TMC Habari**

Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (Gaming Board of Tanzania) Alhamis ya Desemba 04, 2025 imekabidhi rasmi mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na madawati 60 katika Shule ya Msingi Rufu iliyopo Chamazi, Manispaa ya Temeke uliogharimu Shilingi Milioni 50,580,000 za Kitanzania ambapo gharama hizo zimejumuisha ujenzi wa Vyumba viwili vya madarasa na Madawati 60 ya Wanafunzi.




Akizungumza katika Hafla hiyo Mkurugenzi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT) Ndg. James Mbawe amesema Wanafunzi wahakikishe wanatunza Vyema Vifaa hivyo Ili viweze kutumiwa pia na wanafunzi wengine wajao.

Kwa Upande wake Afsa Elimu Taaluma Manispaa ya Temeke Ndg. Salum Lugwaza amesema kuwa wanajivunia ugeni huo na kuupokea vema mradi huo huku akimuhaidi Mkurugenzi wa Bodi kuwa watatunza vifaa hivyo.

"Kiukweli tunajivunia sana juu ya ugeni huu na pia pongezi kwa Mkurugenzi wa Bodi ya Kubahatisha juu ya Mradi huu ambao mmetuletea kiukweli tunajivunia sana kwa kuwa unakwenda kusaidia kupunguza changamoto ya Msongamano wa Wanafunzi madarasani na tutahakikisha tunavitunza kwa Ubora mkubwa Ili vije kuwa manufaa kwa kizazi kingine". Alisema Ndg. Lugwaza

> Tumetumia Gharama kubwa katika kujenga Miundo mbinu hii pamoja na kutoa vifaa hivi kwa ajili yenu hivyo basi niwaombe wanafunzi muhakikishe Vifaa hivi Mnavitunza kwa Usalama mkubwa kwa ajili ya Manufaa ya Baadae".
> **Alisema Ndg. Mbawe**

Msaada huo umetolewa kama sehemu ya jitihada za GBT katika kurudisha kwa jamii (CSR) katika sekta mbalimbali lakini vilevile ni muendelezo wa kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuboresha Elimu Nchini.

GBT imeahidi itaendelea kusaidia jamii kwa kadri inavyowezekana ili kuchangia maendeleo hususani katika Sekta ya Elimu, Afya, Mazingira, Michezo.





**BONDIA FURAHISHA APOKEA BARAKA ZA MEYA TEMEKE KUELEKEA PAMBANO LAKE DHIDI YA PHIRI**

**Na Sadam Ndemo, TMC , Habari**

Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Mhe. Uzairu Abdul Athumani Desemba 24, 2025 ametoa maneno ya Baraka kwa Bondia Hamadi Furahisha kama Mwakilishi wa Tanzania katika Pambano la Ngumi dhidi ya Bondia Hanock Phiri kutoka Malawi linalotarajiwa kufanyika Ijumaa Desemba 26, 2025 Ware House, Masaki Jijini Dar es Salaam.

Mhe. Uzairu amehimiza uungwaji mkono wa Mabondia wa ngumi akisisitiza kuwa kwa sasa ngumi si mchezo tu bali ni fursa ya Ajira kwa Vijana wa Tanzania ambapo pia kwa upande wake ameahidi kutoa ushirikiano wa dhati kwa Wanamichezo wote.

''Tuwaunge Mkono Vijana wa Michezo, Michezo ni Ajira na Temeke tupo vizuri kwenye michezo nenda kaiwakilishe Tanzania". Alisema Mhe. Uzairu

Kwa upande wake Bondia Hamadi Furahisha ametoa shukrani kwa fursa na heshima hiyo na kuahidi kupambana kwa nguvu zote kuiletea heshima Tanzania katika medani za Ndondi kimataifa.



**''Nimekuja kuchukua baraka kwa Mstahiki Meya, nashukuru sana kwa nafasi hii na naahidi kuleta ushindi".** Alisema Bondia HamadI

# DC MAPUNDA ASHIRIKI MBIO ZA POLE

**Na Mwandishi Wetu, TMC Habari**

Mkuu wa Wilaya ya Temeke Mhe. Sixtus Mapunda Oktoba 26, 2025 alishiriki Mbio za pole (Jogging) zilizoanzia Uwanja wa Benjamin Mkapa hadi Hospital ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke m ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za wadau wa maendeleo wanaojitokeza kusaidia Sekta muhimu ya Afya hapa Nchini sambamba na kuhimiza Wananchi kushiriki Uchaguzi Mkuu kwa kujitokeza kwa wingi Kupiga Kura ifikapo Jumatano ya Oktoba 29, 2025.




Akihitimisha mbio katika Hospital ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke DC Mapunda amewataka Wananchi kuendelea kutunza amani iliyopo Nchini hasa katika Kipindi hiki cha Uchaguzi ikiwa ni pamoja na kuepukana na vishawishi vyovyote vinavyoweza kuleta taharuki isiyo na msingi wowote.

Aidha DC Mapunda ametoa Shukrani kwa mdau aliyetoa Vifaa vya kujifungulia jwa Wakinamama Wajawazito vyenye thamani ya takribani ya zaidi ya Milioni 14 za Kitanzania kutoka kwa Kampuni ya PRADLE Medics chini ya Mkurugenzi wake Eliasa Mkongo.

Viongozi Mbalimbali wameshiriki Mbio hizo akiwemo Daktari Joseph Kimaro ambaye ni Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Temeke.





## ZOEZI LA USAFI WA MAZINGIRA KILA MWISHO WA MWEZI

**Na Ramadhani Fupi, TMC, Habari**

Novemba 29, 2025 ikiwa ni Jumamosi ya Mwisho wa Mwezi Viongozi, Wananchi na Wadau mbalimbali wa Usafi wa Mazingira Manispaa ya Temeke wamejitokeza kwa wingi kufanya usafi katika Kata ya Charambe ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya kufanya Zoezi la Usafi wa Mazingira kila ifikapo Jumamosi ya Mwisho wa Mwezi.



Akizungumza na Wananchi kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Mwanasheria wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Ndg. Shafii Mshamu amewapongeza Viongozi, Wananchi na Wadau mbalimbali waliojitokeza kushiriki zoezi la usafi wa mazingira na kuwasihi wananchi kuendeleza utamaduni huo katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kutunza mazingira na Afya.

Nae Balozi wa Mazingira Nchini Ndg.Michael Msechu amekabidhi Zawadi ya Tisheti, Fedha na Mtungi wa Gesi kwa baadhi ya Wananchi akiwemo Mama lishe ambao wameonekana kuwa Vinara wa Usafi kwenye Maeneo yao ya Biashara na kuhimiza Wafanyabiashara wengine kuiga mfano kutoka kwao.



**Tunza Mazingira Yakutunze**




## VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA (CLUSTER) MANISPA YA TEMEKE

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ina Vituo sita vya kutolea Huduma (Cluster) ambavyo ni Buza, Charambe, Chamazi, Tandika, Kijichi na Miburani.

Yote hii ni katika kukusogezea huduma karibu yako ili uweze kupata huduma kwa haraka na kuendelea na shughuli za kujenga Taifa,hakuna haja ya kwenda mbali tena kufuata huduma.

Fika katika kituo kilichopo karibu na wewe upate huduma ikiwemo malipo ya leseni, ushuru wa huduma (service levy), kodi za majengo na ardhi, vibali mbalimbali n.k

Kituo cha Huduma Kijichi kipo Soko jipya Kijichi, Buza kipo Stendi mpya ya Buza, Chamazi kipo Magengeni, Tandika kipo Tandika Sokoni, Char ambe kipo Rangi tatu sokoni, Miburani kipo ofisi za Manispaa ya Temeke.

**"Kwa Pamoja tushirikiane kuijenga Temeke yetu"**



## MAAFISA BAJETI WA IDARA NA VITENGO WANOLEWA JUU YA UANDAAJI WA MIPANGO NA BAJETI.

**Na: Mussa Chisongela, TMC Habari**

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kupitia Idara ya Mipango na Uratibu Novemba 27, 2025 imetoa Mafunzo kwa Maafisa Bajeti kutoka Idara na Vitengo vyote katika Manispaa hii juu ya uandaaji wa  Mipango na Bajeti katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 2025/2026.

Maafisa hao wamepata Elimu juu ya Umuhimu wa uandaaji wa mipango na Bajeti ya Serikali, Asili ya Mpango na Bajeti, Hatua za uandaaji wa mipango na bajeti, Masuala ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa Mipango na Bajeti ikiwemo maelekezo ya mwongozo wa uandaaji wa bajeti unaotolewa kila mwaka na Wizara ya fedha.

Kaimu Mkurugenzi Ndg.Yahya Madenge amefungua Mafunzo hayo kwa kupongeza na kusisitiza Wakuu wa Idara kushirikiana na Maafisa Bajeti kuandaa Bajeti kwa kuzingatia yanayotakiwa katika Idara zao.

"Nawapongeza kwa juhudi hizi ambazo mmezifanya za kukutanisha watu hawa ambao ni wadau muhimu ambao tunawategemea sana katika kutengeneza Bajeti yetu ya Mwaka, Ni matumaini yangu kwa Mafunzo haya mtakwenda kuandaa Bajeti imara kwa kuzingatia Mpango mkakati (strategic planning) wa Idara na Taasisi". Alisema Ndg.Madenge.

Mafunzo haya yanatarajiwa kudumu kwa Siku tatu yakitarajiwa kuwa Nyenzo muhimu kwa Maafisa hao katika Uandaaji wa Bajeti lakini vilevile uingizaji wa Mipango na Bajeti hizo katika mfumo wa Planrep.

Akifunaa mafunzo hayo Ndg. Gervas Lupembe ambaye ni Mkuu wa Idara ya Mipango na Uratibu  Manispaa ya Temeke alisisitiza  Maafisa Bajeti hao kushirikiana na Wakuu wa Idara kuandaa Bajeti kwa kuzingatia Vipaumbele vya Serikali inayoongozwa Chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Miongozo inayotolewa na Wizara, Mpango Mkakati wa Idara na Taasisi pamoja na Mahitaji ya Idara zao husika.

" Ili uweze kufanikiwa jambo lako lazima upange, tunapanga alafu mwisho wa siku tunafanikiwa, Nendeni kwenye Idara zenu mkajadiliane vipaumbele, malengo na shughuli kutokana na Mpango wenu kisha Andaeni Mpango makini utakaozingatia Miongozo niliyoitaja. Andaeni Mipango inayotekelezeka  iliyo sahihi, Shughuli (Activities) ziwe halisi, zifikike, na zipimike kwa kipindi maalumu. "Avoid poor planning". Alisema Ndg. Lupembe

Mafunzo haya yanatarajiwa kuwa Nyenzo muhimu kwa Maafisa hao katika Uandaaji wa Bajeti lakini vilevile uingizaji wa Mipango na Bajeti hizo katika Mfumo wa Planrep.

# MAADHIMISHO YA WIKI YA AFYA YA MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA MANISPAA YA TEMEKE

**Na: Joanita Joseph, TMC Habari**

Ikiwa ni Maadhimisho ya Wiki ya Magonjwa yasiyoambukiza, Manispaa ya Temeke kupitia Idara ya Afya leo Novemba 13, 2025, imetoa Mafunzo kwa Watoa huduma za Afya wanaotoka katika Vituo vya kutolea huduma za Afya vya Umma vilivyopo katika Manispaa hii kwa kuwapatia elimu juu ya namna ya kuchukua taarifa sahihi za Magonjwa yasiyoambukiza na kuzihifadhi katika Mifumo ya ki elektroniki ili kuwezesha ufuatiliaji, utoaji huduma na kuendelea kuboresha Afya zao lakini vilevile kuwezesha halmashauri kuwa na Mipango ambayo ni halisi katika utoaji huduma kwa wagonjwa hao.

Akifungua Mafunzo hayo Mganga Mkuu wa Manispaa ya Temeke Dr. Jonas Lulandala amesema " zaidi ya 75% ya Watu katika Nchi zenye uchumi wa chini na wa kati wanaugua Magonjwa yasiyoambukiza hivyo ni wajibu wetu sisi kama watoa huduma, ni wajibu kwa serikali kuona namna ya kuboresha utoaji huduma kwa watu ambao watakuwa wamepata magonjwa hayo"

Kwa upande wake Mratibu wa Magonjwa yasiyoambukiza Manispaa ya Temeke Bi. Happy Nkunda amesema "Sisi kama halmashauri tumejipanga katika vituo vyetu 31 kutoa huduma za Uchunguzi na Matibabu, tukiadhimisha wiki hii huduma zinatolewa bure katika Vituo vyetu vya Afya hivyo Wananchi wote tunawakaribisha".

Wiki ya Magonjwa yasiyoambukiza imeanza Novemba 10, 2025 huku ikitarajiwa kufikia kilele siku ya jumamosi Novemba 15, 2025.





# VISABABISHI VYA WATOTO KUZALIWA NA UZITO PUNGUFU KUFANYIWA UTAFITI

**Na Ramadhani Fupi, TMC Habari**

Wataalamu wa Afya wanaofanya Utafiti juu ya Visababibishi vinavyopelekea Watoto kuzaliwa na Uzito pungufu katika Manispaa ya Temeke leo Novemba 21, 2025 wamekutana katika Ukumbi wa Afya wa Manispaa kwa lengo la kufanya tathmini ya takwimu zilizokusanywa katika Vituo ili kuboresha zaidi utafiti huo na kuweza kuainisha changamoto yoyote iliyobainika ili iweze kutatuliwa mapema kabla ya kufika mwisho wa utafiti huo.

Bi. Happy Nkunda ambaye ni Afisa lishe wa Manispaa ya Temeke amesema kuwa kupitia Kikao hicho wamewekeana Mikakati ili kuhakikisha kuwa wanapata taarifa sahihi kuhusu watoto wote wanaozaliwa na uzito pungufu ndani ya Manispaa ya Temeke ili kuja na mapendekezo sahihi yatakayosaidia kuandaa Mikakati maalum Kitaifa ili kupunguza au kuondokana kabisa na tatizo hilo.

Kwa upande wao Wataalamu wa Afya walioshiriki kikao hiko wamepongeza hatua iliyochukuliwa na Viongozi wao ya kufanya kikao cha tathmini ya mwenendo wa Utafiti kwa kuwa itawasaidia kupata suluhu ya changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo wakati wa ukusanyaji wa taarifa zao.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE




## Tupo kwenye Mwezi wa Afya na Lishe ya Mtoto.

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kupitia Vituo vyote vya Kutolea huduma za Afya tunaendelea na utoaji wa Matone ya Vitamin A kwa Watoto chini ya Umri wa Miaka Mitano (5). Mzazi Mpeleke mwanao akapate huduma, Kinga ni bora kuliko tiba!


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
TEMEKE
Tuko Tayari
Kushiriki Uchaguzi mkuu 2025
INDEPENDENT NATIONAL ELECTORAL COMMISSION
TANZANIA
Vituo vitafunguliwa Saa 01:00 Asubuhi na kufungwa Saa 10:00 Jioni
"Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura"
@temeke_mc



# MSIMAMIZI WA UCHAGUZI JIMBO LA MBAGALA WAFUNDA MAKARANI WAONGOZAJI

**Na Ramadhani Fupi TMC Habari**

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Mbagala Wakili Fortunata Shija amewataka Makarani Waongozaji Wapiga Kura kusoma Sheria, Kanuni na Miongozo ya Uchaguzi pamoja na kufuata Maelekezo kutoka Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ili kuongeza ufanisi katika Zoezi la Upigaji Kura.



Wakili Shija ameyasema hayo leo Desemba 26, 2025 wakati akifungua Mafunzo ya Makarani Waongozaji Wapiga Kura yaliyofanyika katika Ukumbi wa Iddy Nyundo Manispaa ya Temeke ikiwa ni Maandalizi kuelekea Siku ya Uchaguzi wa Marudio Nafasi ya Udiwani utakaofanyika Jumanne ya Desemba 30, 2025 .

" Pamoja na uzoefu mlionao,  msiache kusoma katiba, sheria, kanuni, taratibu na maelekezo yote yanayotolewa na Tume". Alisema Wakili Shija

Kadhalika Wakili Shija amewashukuru Makarani wote waliojitokeza kwenye Mafunzo hayo na kuwatakia kazi njema katika majukumu yao ya kulitumikia Taifa.

**"Kura Yako Haki yako Jitokeze Kupiga Kura"**

# TUFUATILIE KUPITIA MITANDAO YA KIJAMII



→ @temeke_mc

Au Tembelea Tovuti yetu
www.temekemc.go.tz



Jarida hili hutolewa na
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Manispaa ya Temeke
S.L.P 46343, Temeke, Dar es Salaam

**Simu:** +255 22-2928132
**Nukushi:** +255 22-2928137
**Barua pepe:** temeke@temeke.go.tz
**TOVUTI:** www.temekemc.go.tz

Kusoma au kupakua toleo
lililopita la Jarida hili Tembelea
**www.temekemc.go.tz**
au Scan hapa